**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

**SamsKleJah, Musician (Burkina Faso)**

Author: Susanne Fuchs

Editor: Stefanie Duckstein

Translation: Anthony Dunham

Sound clips in DALET: Learning by Ear – LBE_PEO_Musician_xxx

CHARACTERS:

Announcer: female voice

SamsKleJah, musician (male, 38)

Sylvestre Ouédraogo, tradesman (male, 20)

Yacine Sama, daughter of SamsKleJah (female, 10)

Geoffrey Darakoum, student (male, 23)

INTRO

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina Watu wanaoleta mabadiliko. Katika vipindi hivi utapata fursa ya kuwafahamu mashujaa wanaojulikana na wale ambao hawajulikani barani Afrika. Watu hao ni mashujaa, wa kweli - wamejitolea na wangependa kubadilishana nawe mawazo kuhusu haki na utulivu duniani, kwa imani kuwa upo uwezekano wa mabadiliko mema. Leo hii tunakutana na SamsKleJah, mwanamuziki wa Reggae kutoka Burkina Faso. Yeye ni shujaa wa kila siku kwa vijana wengi wa Afrika Magharibi.

**TEXT:**

1. *SFX: Car (constant background sound of a car's motor)*

Tunasafiri kwenye motokaa pamoja na SamsKleJah kupitia mji mkuu wa Burkina Faso, Ouagadougou. SamsKleJah, mwenye umri wa miaka 38 jina lake hasa ni Karim Sama, anafurahi kwa sababu wimbo wake mmoja unachezwa kwenye radio. Kuna joto kali katika mji wa Ouagadougou. Madirisha ya gari yako wazi na, SamsKleJah anaimba kwa sauti kubwa, kufuatisha wimbo wake. Pembeni mwa barabara vijana wanamtambua na wanampungia mkono huku wakitabasamu.

2. *SFX: SKLJ is singing (sound remains down)*

SamsKleJah anajulikana nchini Burkina Faso na kwengineko. Sio tu kwa muziki wake wa Reggae bali kwa sababu ya kipindi chake cha radio cha kila wiki kinachoitwa "Roots, Rock, Reggae" ambacho kinasikika moja kwa moja nchini kote au hata kupitia kwenye kaseti na CD zilizorekodiwa..

3. *SFX: Excerpt from „Roots, Rock, Reggae"*

Hachezi muziki wa Rock na Reggae pekee kwenye shoo yake bali yeye huzungumzia mambo yanayohusu maisha kwa jumla. Vijana kwa wazee wanamsikiliza hasa pale anapokosoa maisha ya kileo na kutoa ushauri. Mara nyingine huwa na wageni kwenye studio ijapokuwa mara nyingi yeye huwa peke yake na wala haogopi kusema waziwazi mambo yanayotokea. Kukosoa kwake

hakuwalengi tu wanasiasa fisadi walio madarakani. Kila mara anakumbusha kuwa kuwajibika na kuwa muadilifu ni vitu ambavyo huanzia chini kabisa.

4. *SFX: Car door, footsteps*

Anaelezea ni kwa nini mara tu anapofika nyumbani:

5. *Sound Clip SamsKleJah*

*“Kila mtu anapaswa kuelewa kwamba anaweza kubadili mambo, kila mtu anapaswa kuelewa kuwa yeye ni muhusika katika mnyororo huo.  Kila mtu ana tofali ambalo anaweza kuchangia katika ujenzi huu.  Pindi kila mmoja wetu atakapo fahamu hilo basi tutakuwa tumepata mafanikio.“*

SamsKleJah anatilia mkazo sana wakati anapotoa ujumbe kuwa kila mtu anastahili kuwajibika juu ya maisha yake na wala mtu asivunjike moyo.

6. *Sound Clip SamsKleJah*

*“‘Kwa muda mrefu sasa ninarudia ujumbe huo kwenye shoo zangu kwa ajili ya vijana. Nelson Mandela ni mwananadamu na mimi pia naweza kuwa Nelson Mandela. Barack Obam ni mwanadamu na mimi pia ninaweza kuwa  Barack Obama. Na hivyo ndivyo haswa unavyopaswa kufikiria wakati ukiamka kila siku asubuhi. Kabla hujaenda kulala unahitaji kuiangalia siku yako nzima jinsi ulivyo ipitisha. Jiulize, Je, leo nilifanya kitu ambacho kimenifaidi mimi mwenyewe pamoja na watu wengine?  Hicho ni kipima joto changu mimi.  Nina maana hata mimi ninaweza kuwa kama mmoja wao kwa sababu  hata wao hawana vichwa viwili au mikono minne. Sisi sote tuko sawa ila kinachotofautisha hapa ni mtu kuwa na uwezo wa kujishurutisha kufanya mambo. Vinginevyo sote tuko sawa.”*

7. *SFX : Grand Marché de Ouaga (let the sound run under the text)*

Katikati ya soko mjini Ouagadougou – kila mahala wafanyabiashara na akinamama wachuuzi wanajaribu kuuza bidhaa zao. Kelele na fujo kama ilivyo kawaida katika soko lolote kubwa. Sylvestre Ouédraogo anauza bidhaa zilizotengenezwa kwa mikono. Lakini ifikapo siku ya Ijumaa saa mbili usiku yeye husimamisha kila kitu kwa ajili ya kusikiliza shoo ya SamsKleJah'. Shoo hii huwa muhimu sana kwake hasa ikiwa siku yake ilikuwa ngumu na amechoshwa na mambo.

8. *Sound Clip Sylvestre Ouédraogo*

*"Binafsi nafurahishwa sana na shoo zake wakati ninapokuwa nimetafshika, basi husikiliza kipindi chake na huwa ananiliwaza sana. Mtu ukizidiwa na wasiwasi basi huwa hujui la kufanya, lakini ukisikiliza anavyosema unaona kuwa unapata faraja ya kuendelea na maisha.*

SamsKleJah haanzi shoo yake na hamjambo mabibi na mabwana, Hapana yeye husema Hi! Kina kaka na Kina dada mashujaa! Kuwakumbusha wasikilizaji wake kuwa wanatakiwa kuendelea kupambana kila wakati. Lakini je ana maana gani kwa kusema mapambano? Unadhani mapigano? Au vita vya silaha? La, ni jambo jingine tofauti kabisa anaeleza Sylvestre:

9. *Sound Clip Sylvestre Ouédraogo*

*"Kupambana kuna maana kuwa kila mara unakuwa na mawazo ya kujiendeleza yaani kuamini kwa kila utakachokuwa unakifanya ambacho kinasogeza gurudumu la maendeleo ya nchi mbele. Kufanya mambo ambayo yanaleta*

*maendeleo kwa binadamu na pia kuiendeleza Burkina yetu, Afrika yetu. Hivyo ndivyo mimi ninavyoelewa.“*

*10. SFX (slowly fade in concert excerpt )*

‘Hivyo ndivyo maisha yalivyo ’ SamsKleJah anaimba kwenye tamasha la kusherehekea miaka kumi ya shoo yake ya radio. Kuna kupanda na kushuka lakini hupaswi kuvunjika moyo kwa lolote lile, naye anafahamu fika kwa hilo analolisema kwani hata yeye maisha yake hayakuwa rahisi hivyo! Amekumbana na hali nyingi katika maisha zilizompa uoga na mitihani maishani.

*11. Sound Clip SamsKleJah*

*”Hata mimi nina matatizo, saa zingine mimi hujificha ili nipate kulia kwa sababu huwa nimekumbwa na jambo gumu, kwa sababu huwa nimehuzunika au kwa sababu, kwa sababu, kwa sababu …”*

Mara zote yeye hufikiria kuwa jambo la muhimu ni Usikate tamaa, Usivunjike Moyo ila ukubali changamoto katika maisha. Anacheka anapokumbuka alipotangaza kwa mara ya kwanza mwezi Juni mwaka 1999

*12. Sound Clip SamsKleJah*

*“Ulikuwa ni ubatizo kwangu. Nilifika studio lakini sikuwa nimewahi kuzungumza kwenye maikrofoni hata siku moja. Siku hiyo nilikuwa nimeandika kila kitu nilichotaka kukisema lakini nilikuwa ninatetemeka na moyo wangu ulidunda kwa haraka. Basi nilipofanya shoo yangu mara mbili, tatu hivi nilianza kujiamini. Siku moja nilipofika kwenye kituo cha utangazaji nilikuta barua na ilikuwa inatoka kwa msikilizaji ambae alinipongeza kwa kazi yangu, hapo nilifahamu kuwa watu*

*walikuwa kweli wananisikiliza!*

Na huo ndio ulikuwa mwanzo wa kazi yake ya utangazaji. Leo hii yeye sio tu mtangazaji mwenye shoo yake inayojulikana bali yeye pia ni mkuu wa vipindi na naibu mkurugenzi wa kituo maarufu cha matangazo ya radio nchini Burkina Faso. Ana mtoto mmoja wa kike mwenye umri wa miaka 10 anaitwa Yacine, anasoma mjini Ouagadougou. Yacine anaelewana vizuri sana na baba yake, yeye huimba pamoja na baba yake kwenye matamasha mbali mbali.

*13. SFX Playing boules in the country*

Ni wikendi na Yacine na baba yake wamesafiri kidogo kwenda mashambani. Ni jambo la kawaida kwa SamsKleJah kuandaa safari kama hizi kwa watoto na vijana kwa sababu yeye hupenda kuwatoa vijana kutoka kwenye maeneo ya jiji ambayo mazingira yake yamechafuka. Wakati huu lakini Yacine amesafiri na baba yake tu na anamuangalia akicheza mtindo wa taratibu (boules).

*14. SFX Playing boules in the country*

Anamfahamu baba yake nje ndani na anajua kinachomkasirisha baba yake pia.

*15. Sound Clip Yacine Sama*

*“Hapendi watu wakisengenyana. Anapenda watu wakiheshimiana. Kisichokubalika kabisa ni wizi, Ubakaji au Kuua. Bidhaa kuuzwa ghali mno na watu masikini kukosa mahala pa kuishi yote hayo hayakubaliki.”*

Yacine pia anafahamu kile baba yake anachokipigania:

*16. Sound Clip Yacine Sama*

*‚Aliniambia kuwa anapigania haki kwa wote.'*

Mjini Ouagadougou, Geoffrey Darakoum anatafakari kwa nini SamsKleJah ni mtu muhimu. Geoffrey, ana umri wa miaka 23, ni mwanafunzi wa masomo ya Biashara wa mwaka wa tatu katika chuo kikuu ambae ni msikilizaji wa kipindi cha SamsKleJah kwa miaka kumi.

*17. Sound Clip Geoffrey Darakoum*

*"Mwanamuziki wetu SamsKleJah ni mfano wa kuigwa na vijana wa Burkina. Ni yeye tu hapa nchini ambae haogopi kusema ukweli, nyimbo zake ni kichocheo kwa jamii kuwa na mtazamo wa kidemokrasia, haki na usawa. Haki kwa Wote!"*

Kwa sababu wale ambao wanaitambua na kuijua haki yao ndio wanaoweza kuidai.

*18. Sound Clip Geoffrey Darakoum*

*"Sisi tunasema huwezi kupata kitu chochote kama hukiombi."*

Hii ndio sababu SamsKleJah kila mra husema kwenye kipindi chake kwamba katika nchi yenye haki za kiraia, watu wote wana haki sawa na kwamba sheria lazima imlinde kila mtu, kila kosa lazima litolewe hukumu bila kujali ni nani amefanya kosa hilo. Na jambo moja la muhimu sana ambalo anawasisitizia vijana ni.

*19. Sound Clip SamsKleJah*

*'Lazima muulize maswali mengi kwani hiyo ndio njia pekee ya kujifunza na kuelewa mambo. Kama Bibilia isemavyo Kilichojificha kutoka kwa wahenga kitaletwa mbele ya mwanga na watoto, kwa hivyo ni lazima watoto waulize maswali mengi...mengi tu!*

*(Laughter)*

OUTRO

Huo ulikuwa ni wasifu wa SamsKleJah, mwanamuziki shupavu wa Reggae na mtangazaji wa radio anayetoa maoni yake bila woga. Yeye ni kioo cha jamii na shujaa kwa vijana wengi nchini Burkina Faso na nchi jirani. Anawahimiza vijana wasikate tamaa wanapokumbwa na shida mbalimbali na pia anaikumbusha jamii juu ya umuhimu wa kuwajibika ili kuufanya ulimwengu kuwa mahala pazuri. Je umefurahia kipindi hiki? Iwapo ungependa kututumia maoni yako, jielimishe zaidi kuhusu yale yaliyozungumzwa leo hii au kisikilize tena kipindi hiki. Anuani ya mtandao wetu ni www.dw-world.de/lbe. Asante kwa kutusikiliza sina shaka utaungana nasi tena wakati mwingine ili kusikiliza hadithi mpya katika makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu watu wanaoleta mabadiliko. Kwaheri kwa sasa!